

## BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1

Fax Nam. + 255 24 2230215

Tovuti: [www.zanzibarassembly.go.tz](http://www.zanzibarassembly.go.tz)



SANDUKU LA BARUA 902,

ZANZIBAR

Barua Pepe: [zahore@zanlink.com](mailto:zahore@zanlink.com)

### HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA KUREKEBISHA SHERIA MBALI MBALI NA KUWEKA MASHARTI BORA NDANI YAKE, 2021

**Mheshimiwa Spika**, kwanza kabisa naanza kuwasilisha Hotuba yangu hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehema, Muumba wa Mbingu na Ardhi na vyote vilivyomo kwa kutujaalia uhai na afya njema ambayo imetuwezesha kutekeleza majukumu yetu. Ninamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu Azidi kutujaalia amani na upendo, busara na hekima, pamoja na neema zake zote ambazo ni muhimu sana katika maisha yetu.

**Mheshimiwa Spika**, Napenda pia, kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Hotuba ya maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa katika Mkutano huu wa Nne wa Baraza hili tukufu katika kuuchangia na kuuboresha Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbali Mbali na Kuweka Masharti Bora Ndani Yake. Tunamuomba Mwenyezi Mungu akuzidishie hekima na busara katika kutekeleza majukumu yako ya kila siku.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, pongezi za dharti kabisa ziende kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Dkt. Mwinyi Talib Haji pamoja na watendaji wote wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar kwa ushirikiano wao mkubwa kwa Kamati wakati Kamati ilipokuwa ikijadili Mswada huu, pamoja na watendaji wa Divisheni ya

Ushauri wa Kisheria kutoka Afisi ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar kwa kuipatia taaluma Kamati yetu lakini vile vile, tunaomba utoaji wa taaluma uwe endelevu na ni vyema Wajumbe wote wa Baraza wakapatiwa taaluma hii ya kutunga sheria ambapo itasaidia kwa Wajumbe kuwa wataalamu na itatoa fursa kwa Wajumbe kutekeleza miongoni mwa majukumu yao ya Kikatiba ya kutunga sheria kama ilivyoielezwa katika kifungu cha 88 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984.

**Mheshimiwa Spika**, pia, shukurani za pekee ziende kwa Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mashirikiano yao makubwa waliyotoa kwangu na juhudi zao wakati wa kuujadili kwa kina Mswada huu.

Naomba sasa kwa ruhusa yako niwatambulishe Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa majina kama ifuatavyo:

1.	Mhe. Hassan Khamis Hafidh	Mwenyekiti
2.	Mhe. Mtumwa Peza Yussuf	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Machano Othman Said	Mjumbe
4.	Mhe. Suleiman Makame Ali	Mjumbe
5.	Mhe. Salma Mussa Bilal	Mjumbe
6.	Mhe. Mohammed Mgaza Jecha	Mjumbe
7.	Mhe. Zaina Abdalla Salum	Mjumbe
8.	Ndg. Haji Jecha Salum	Katibu
9.	Ndg. Salma Muhsin Haji	Katibu
10.	Ndg. Amina Abeid Hemed	Mkalimani

**Mheshimiwa Spika**, sina budi kueleza kuwa, Mswada huu ni marekebisho ya baadhi ya vifungu katika sheria mbali mbali ambapo vingi kati ya vifungu hivyo vinafanyiwa marekebisho ya kuvirudisha katika sheria zao za awali baada ya Serikali kuondoa ugatuzi. Hivyo, maelezo zaidi ya mapendekezo hayo yanaonekana katika Marekebisho ya Kamati ambayo Waheshimiwa Wajumbe tayari mmeshapatiwa kwa ajili ya ufafanuzi na ufahamu zaidi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri katika kifungu cha 7, kufutwa na kuandikwa upya kifungu kipya cha 11A ili kiweze kuakisi madhumuni yaliyokusudiwa kama ifuatavyo:

*“11A. Kunaanzishwa diko, ikiwa kuna ulazima, katika kijiji kilichopo kwenye ukanda wa mwambao ndani ya Zanzibar ambalo litaainishwa na Idara kwa kushirikiana na taasisi husika za Serikali na litamilikiwa na Wizara”.*

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 11(2) kinashauriwa kurekebishwa kwa kuongezwa maneno *“kwa mwalimu mkuu wa”* baina ya neno *“itawasilishwa”* na *“skuli”* kwa ajili ya kuainisha muhusika halisi atakayekebidhiwa Ripoti iliyoelezwa katika kifungu hiki.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, nina imani kwamba Wajumbe wa Baraza hili Tukufu watakubaliana na maoni yote ya Kamati katika Mswada huu kwa lengo la kuiwezesha Serikali kuzifanyia marekebisho Sheria hizi.

**Mheshimiwa Spika**, vile vile, Kamati yetu inawaomba Wajumbe wa Baraza hili Tukufu waujadili na kuuchangia ipasavyo Mswada huu na hatimae kuupitisha ili kuwa sheria ambayo itaziwezesha taasisi hizi kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika,

Naomba Kuwasilisha.

Ahsante,

A handwritten signature in black ink, consisting of several loops and strokes, positioned above a horizontal dotted line.

(Hassan Khamis Hafidh)

Mwenyekiti,

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,

Baraza la Wawakilishi Zanzibar